



## TAMKO LA HAKIELIMU KUHUSU VITENDO VYA UKATILI SHULENI

Tumepokea kwa mshtuko na masikitiko makubwa taarifa za tukio la adhabu ya kikatili aliyopata mwanafunzi aitwaye Sebastian Chinguku wa Kidato cha 3 katika Shule ya Sekondari ya kutwa ya Mbeya. Tukio hili limetusikitisha zaidi baada ya kuona ukatili huu uliopitiliza kuwa unafanywa na walimu tarajali ambao tayari wamepitia mafunzo ya ualimu yanayohusisha pia malezi bora ya wanafunzi wao.

Tunaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za awali zikiwemo kuliagiza jeshi la polisi nchini kuchukua hatua za haraka dhidi ya walimu waliohusika katika tukio hili. Aidha, tunampongeza Mwalimu aliyethubutu kukemea na pia kufichua ukatili huu uliopitiliza. Tunaomba mamlaka husika zichukue hatua madhubuti za kulinda ajira na hata uhai wa mwalimu huyu jasiri.

Pamoja na hatua hizi za awali zilizochukuliwa, HakiElimu inaitaka Serikali kuhakikisha suala hili linashughulikiwa kwa upana wake na kuendelea kuitaarifu jamii juu ya hatua zilizochukuliwa dhidi ya walimu waliohusika na ukatili huu. Ni matumaini yetu kuwa Serikali itaendelea kulishughulikia suala hili kwa uwazi na haraka tofauti na siku za nyuma ambapo imekuwa ikiunda Tume ambazo uchunguzi wake huchukua muda mrefu na matokeo yake pengine kutokuwekwa bayana.

Lakini pamoja na kuwa tukio la Mbeya linaonekana kuchukua mjadala mpana hapa nchini kwa sasa, tunapenda kuikumbusha Serikali kuwa matukio ya ukatili dhidi ya wanafunzi yamekithiri katika shule zetu kwa muda mrefu. Mathalani, Ripoti ya utafiti ya Unicef kuhusu ukatili dhidi ya watoto wa mwaka 2011 imeonesha kuwa kuna viwango vya kutisha vya ukatili dhidi ya watoto katika shule nyingi nchini vikiwemo vya kimwili, kingono na kihisia katika mazingira ya shule za Tanzania na kwamba walimu ndio vinara wa ukatili huo. Kwa mujibu wa utafiti huo zaidi ya nusu ya wasichana na wavulana ambao wamewahi kunyanyaswa kimwili (kufinywa, kuchapwa viboko, na mateke) waliwataja walimu kuwa ndio wanyanyasaji wakuu shuleni nchini Tanzania.

Kwa kiasi kikubwa matukio kama haya yamezifanya shule kutokuwa sehemu rafiki na salama kwa wanafunzi na hivyo kuwa na athari kubwa katika juhudi zao za kujifunza.

Adhabu kama hizi zinapotolewa kwa watoto, husababisha mtoto kutafuta namna ya kukwepa adhabu hizo, ndipo huanza kukosa shule mara kwa mara na hatimaye kuamua kuacha shule kabisa. Hapa tunazidi kubomoa kuliko kutafuta mbinu za kujenga.

Registration  
No. 40897

Board of Directors  
Martha Qorro  
Peter Maduki  
Helen Kijo-Bisimba  
Elinisaidie Msuri  
Rustica Tembele  
Japhet Makongo  
John Kalage

enabling citizens to make a difference in education and democracy

Aidha, matendo haya yamechangia kwa kiasi kikubwa watoto wengi hususani wa jinsia ya kike kuacha shule hivyo kukosa haki yao ya msingi kupata elimu

Kutokana na hali hii, HakiElimu inapendekeza yafuatayo:

1. Serikali ihakikishe kuwa miongozo yake ya kusimamia na kuimarisha nidhamu shuleni inazingatiwa na watu wote.
2. Serikali inapaswa kuanzisha mifumo rasmi ya kutoa taarifa dhidi ya matukio ya ukatili yanayoendelea katika shule zetu itakayowawezesha wanafunzi na wadau wengine kutoa taarifa mara wanapokutana na matukio ya kikatili kama haya katika maeneo yao kwa lengo la kuyakomesha.
3. Serikali iangalie upya utaratibu wa uchaguzi na uandaaji wa walimu katika vyojo mbalimbali vinavyotoa mafunzo ya ualimu hapa nchini kwa lengo la kubaini mapema walimu tarajali wasiofaa.
4. Serikali iweke mipango endelevu itakayolenga kujenga maadili ya walimu walioko kazini juu ya malezi na usimamizi wa wanafunzi wao. Hii ni pamoja na kuishirikisha jamii katika malezi ya watoto.
5. Kamati na bodi za shule na jamii kwa ujumla zisaidie kuhakikisha kuwa shule zinaheshimu na kulinda haki na utu wa wanafunzi.
6. Wazazi, jamii na wadau wengine zikiwemo taasisi za kidini zishiriki kikamilifu katika kuimarisha malezi na kutoa mafunzo ya maadili mema katika jamii ikiwemo umuhimu wa kuheshimu haki za watoto na kuwalinda dhidi ya vitendo vya ukatili.
7. Wanafunzi pia wana wajibu wa kuhakikisha kuwa wanaheshimu walimu pamoja na walezi. Ukosefu wa nidhamu kwa wanafunzi husababisha hali ya kutokuwa na maelewano na upendo kati ya walimu na wanafunzi.



**John Kalage**  
**Mkuregenzi Mtendaji**